



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO



TANGAZO

TANGAZO LA KAZI YA USAFIRISHAJI WA MORAMU, MAWE MCHANGA
NA UUZAJI WA KOKOTO (LOCAL MATERIALS)

NUKUU YA BEI
NAMBA LGA/005/2020/2021/CHUO/US/ 1 LOT 1-5

KWA AJILI YA KAZI YA UJENZI WA CHUO CHA UALIMU

TAREHE 24, DISEMBA, 2020

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imepokea fedha kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa chuo cha Ualimu Ngorongoro katika Wilaya ya Ngorongoro fedha hizi zitatumika katika ujenzi wa majengo na miundombinu ya chuo cha Ualimu Ngorongoro. Njia ya ununuzi itakayotumika wakati wa Ujenzi ni Force Account kwa kuzingatia maelekezo ya matumizi kwa mujibu wa kanuni na.167 ya ununuzi wa umma ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ngorongoro chini ya sheria ya manunuzi ya umma Na.7 ya mwaka 2011 kanuni Na.181 anawatangazia wananchi, makampuni ya usafirishaji na taasisi mbalimbali kuomba kazi za usafirishaji wa Moramu, Mawe, Mchanga na ununuzi wa kokoto katika ujenzi wa chuo kipya cha ualimu Ngorongoro (local materials) zinazohitajika ni kama ifutavyo;

LOT 1. MORAMU (4.5 CUBIC METRES) TRIPS 63
LOT 2. MCHANGA (4.5 CUBIC METRES) TRIPS 530
LOT 3. MAWE (4.5 CUBIC METRES) TRIPS 149
LOT 4. KOKOTO $\frac{3}{4}$ " (4.5 CUBIC METRES) TRIPS 63
LOT 5. KOKOTO $\frac{1}{2}$ " (4.5 CUBIC METRES) TRIPS 149

MASHARTI YA MWOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania
- Waombaji wawe wamesajiliwa na mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA)
- Muombaji awe na leseni hai ya kazi ya usafirishaji
- Kamati ya manunuzi ya ujenzi wa Chuo cha Ualimu Ngorongoro hailazimiki kukubali kima cha juu au cha chini cha bei ya mzabuni

- v. Muombaji awe na risiti ya kielektroniki ya kupokelea malipo(kukiri mapokezi ya fedha)
- vi. Muombaji aambatanishe uthibitisho wa uzoefu aliyo nao wa kazi za usafirishaji
- vii. Kwa wauzaji wa kokoto aoneshe lori la cubic 4.5 atajaza kwa siku ngapi ,wenye clusher ndogo watapewa kipaumbele
- viii. Muombaji aoneshe bei ya kila tripu ya cubic metre 4.5
- ix. Awe na mtaji wa kutosha kwa maana ya rasilimali watu na vitendea kazi muhimu
- x. Maombi yote yaambatanishwe na barua ya maombi ya kazi yenye taarifa ya njia za mawasiliano kama vile namba za simu, barua pepe au anwani za makazi
- xi. Mwombaji ahakikishe fomu ya dhamana ya zabuni imejazwa kwa uhakika bila kukosewa
- xii. Mwombaji ahakikishe fomu zote za maombi ya zabuni zimejazwa kwa uhakika bila kukosewa
- xiii. Vitabu vya nyaraka za nukuu za bei vinapatikana katika ofisi ya Mkuu wa kitengo cha manunuzi ya umma, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.
- xiv. Maombi ya barua yaambatane na risiti ya malipo za maombi ya kitabu cha zabuni Tshs 50,000/=kwa kila ombi la zabuni,kupitia Control namba inayopatikana katika ofisi ya Mweka Hazina wa **Halmashauri (Mawasiliano 0784598490/0767568394)**
- xv. Maombi yanatakiwa kutumwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kuonesha aina ya zabuni inayo ombwa bila kuwa na viashiria vyovyote vinavyoonesha inakotoka na yatumwe kwa anuani ifutayo;

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO
S.L.P 1,
LOLIONDO

Nyaraka za nukuu za bei zinapatikana katika ofisi ya katibu wa kamati ya manunuzi, Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 4/01/2020 saa 5.00 asubuhi na zabuni(nyaraka za nukuu za bei) zitafunguliwa saa 5.30 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro .Waombaji au Wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi



PETER JUMA LEHHET
Kny MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NGORONGORO